Mtazamo Dhidi Ya Kifo na Umilele

(Attitude Towards Death And Eternity)

Na

Ellis P. Forsman

Mtazamo Dhidi Ya Kifo na Umilele

(Attitude Towards Death And Eternity)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 6, 2011

Mtazamo Dhidi Ya Kifo na Umilele

Waeb. 9:27

Mtazamo sahihi kwa hakika huwa ni mizuri. Ni muhimu hasa katika kusanyiko la mahali pamoja.

Tumejifunza mtazamo wetu dhidi ya Mungu, Yesu Kristo, Injili, Kanisa, ndugu zetu wa Kiroho, sisi wenyewe, na ulimwengu; sasa tutajifunza mtazamo wetu dhidi ya kifo na umilele.

Kufika mbinguni, mji wa nafsi zenye haki, mtu lazima apitie njia ya kifo. Hakuna njia nyingine. Kifo ni ahadi isiyoepukika. Waeb. 9:27*, "Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja na baada ya kufa hukumu."*

Maisha katika ulimwengu huu kimsingi imejazwa na ahadi, lakini ahadi nyingi hizo hazijatimizwa. Hataivyo, kuna ahadi moja tu, kwamba kila mtu aliyezaliwa katika ulimwengu huu lazima aitimize. Siyo swala la kuisahau; na wala siyo swala la uchaguzi. "*...watu wanavyowekewa kufa mara moja...*"

Ni nini mtazamo wetu kuhusu kifo?

Watu wanapokumbana na ujio wa kifo uamzi wao dhidi yake unakuwa mkubwa, inategemea kwamba ni wakristo, au si wakristo. Mtu wa ulimwengu, mara nyingi kama si hakuna, anaweza kuchagua kutokufikiria kifo hata kidogo.

Yohana Wayne, akiwa na miaka 71, alieleza kwamba wakati mwingine anakuwa na wakati mgumu akiangalia video zake za zamani: "Ni kama inatisha kuona kwamba nilikuwa na mtazamo mzuri nilipokuwa na umri wa miaka 40, na ghafla naweza kutazama na kuona hii miaka 71 — sing'ai — nataka kuwepo kwa muda mrefu."

Woody Allen wakati Fulani alisema hivi, "siyo kwamba naogopa kufa. Ni kwamba tu sitaki kuwa pale ambapo kifo kinatokea."

Leo, uoga wa baadhi ya watu dhidi ya kifo imeongezeka na inanguvu sana na ujasiri wao katika teknologia umekuwa mkubwa kwamba wanatumia makumi ya maelfu za dola ili kuwezesha miili yao ikaushwe wakati wa kufa. Tarajio lao ni kwamba wanaweza kupokelewa tena ili waweze kuishi tena wakati tiba ikipatikana ya kile kilicho sababisha kifo chao.

Mkristo anaangalia kifo kama mlango wa njia iongozayo katika uzima mkuu ambayo Mungu ametunza kwa ajili ya waaminifu. Wale Wakristo wanaobaki nyuma hawauzuniki kwa sababu nafsi imepotea, bali kwa sababu mpendwa atakoswa sana mpaka wakikutana tena.

Watu wengine katika kupotea kwa mpendwa wao katika familia wanakuwa na maombolezo mengi kwa siku nyingi, majuma, na hata wakati mwingine miaka. Si afya kwa mtu kuacha akilizao kuendela kufikiria kwa kupoteza kwao.

Mtazamo Wa Paulo Dhidi Ya Kifo

Wafil. 1:21-24, *"Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida. Ila ikiwa kuishi katika mwili, kwangu mimi ni matunda ya kazi, basi nitakalolichagua silitambui. Ninasongwa katikati ya mambo mawili; ninatamani kwenda zangu nikae na Kristo maana ni vuzuri sana; bali kudumu katika mwili kwahitajiwa zaidi kwa ajili yenu."*

Katika kifungu hiki Paulo alishikwa na bumbuwazi – alishikwa na chaguzi mbili kuu uzima au kifo. Lakini alijianda kwa vyote.

Maneno ya kifungu hiki si maneno ya Mkristo mpya aliyezaliwa, lakini ni lugha ya mtu aliyekomaa katika Kristo.

Paulo alikuwa na hamu tatu ambazo anaeleza katika barua yake kwa Wafilipi:

Kukutwa katika Kristo

Wafil. 3:9, *"Tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani."*

Kumuadhimisha Kristo

Wafil. 1:20, *"Kama vile nilivyotazamia sana na kutumaini kwamba sitaaibika kamwe, bali kwa uthabiti wote, kama siku zote na sasa vivyo hivyo Kristo ataadhimishwa katika mwili wangu, ikiwa kwa maisha yangu, au ikiwa kwa mauti yangu."*

Kuwa pamoja na Kristo

Wafil. 1:23, *"Ninasongwa katika ya mambo mawili, ninatamani kwenda zangu nikae na Kristo maana ni vuzuri zaidi sana."*

Wakati Wa Kifo Ni Ghafla

1 Sam. 20:3, "*...lakini ni kweli aishivyo BWANA, na iishivyo roho yako, iko hatua kati ya mimi na mauti.*"

Hata mtu akiishi katika ulimwengu huu siku moja, au miaka mia moja, kuna hatu moja tu katika chumba cha kifo.

Kifo kinaweza kikawa kizuri. Kwa mwana wa Mungu mwaminifu, kifo ni zoezi la hitimisho, na kukamilika na yaliyopita na mwanzo umilele usioisha wa furaha, amani, na furaha iliyojaa.

Kifo Cha Ulimwengu Mzima

Kifo ni cha ulimwengu mzima. Kila saa ya kila siku marazote kifo kinatuzunguka.

Uthibitisho wa kifo kiasili wakati mwingine inakuwa nzuri.

Uwa zuri linaweza likawa zuri katika uzuri wake wote na manukato mazuri ambayo yatokea hewani, wakati inanyaukia katika kifo.

Mtu anatakiwa tu aendeshe hadi milimani, zaidi sana katika Uingereza mpya, katika miinuko kuona rangi zuri ya mamilioni ya matawi yanayo kufa ya miti, kila moja inatoa rangi yake, na inaonyesha ujumla ya uumbaji wa Mungu.

Tutaishia kama matawi.

Kwa kawaida, mti mkubwa hauwezi kuisha kwa maramoja. Baadhi huisha na kufa wakati wa kiangazi na mengine yana sitawi. Mengine yakufa wakati wa masika. Mengine yana nyauka na kuanguka wakati wa mvua za vuli.

Ni jinsi gani alivyokuwa makini nabii wa Mungu Isaya 64:6, "*...na wote tutaisha kama matawi;...*"

Wengi ambao hawajakomaa wanatolewa wakati bado wanapendwa, kabla bado hawaja kuwa katika ujana. Au baadhi ya vijana wa kike na wa kiume wanaisha kabla ya wakati wa kiangazi cha maisha. Kuna wale walioishi muda mwingi wa maisha na kuisha na kuanguka wakati wa vuli wa maisha yao.

Hakuna mtu anayejua maisha yake yatakuwaje.

Matawi yanaanguka kimyakimya.

Moja kwa moja zinatoa rangi zao na kuanguka, lakini mtu anayeweza kueleza maendeleo ya maisha yao na kifo kwanzia mwisho na mwanzo.

Ndivyo ilivyo kwa mwanadamu. Hakuna ukaribu ambao mtu anaweza kuishi kwa karibu wakati akianza kuishi.

Wengi wetu tunafikiria kuhusu kifo kama kiko mbali nasi, lakini haipo mbali. Mtu anaanza kufa wakati akianza kuishi.

Kifo, tunavyoifikiria, ni hatua chache kutoka mahali ambapo mtu anaweza kukanyaga kutoka katika ulimwengu huu hadi katika hatua ya milele.

Wakati mtu akiondoka katika ulimwengu huu, anaacha mwili wake wa nyama. Mwili wake ambao siyo wa nyama inatoka nje ya huu mwili wa nyama na siku Fulani *"Kuvaa kutokuharibika".* 1 Wakor. 15:54-55*, "Basi huu uaribikao utakapovaa kutokuharibika, na huu wa kufa kutakapovaa kutokufa, hapo ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikwa, mauti imemezwa kwa kushinda. Ku wapi, ewe mauti, kushinda kwako? U wapi ewe mauti uchungu wako?"*

Nafsi (Roho) Ya Mtu Haifi

Katika mwanzo kabisa, Biblia inasema kuwa Mungu alimpulizia mwadamu pumzi ya uzima na mwanadamu akawa *"nafsi hai".*

Tumaini la mbinguni litakuwahalipo kama nafsi ya mwanadamu itakufa. Yoh. 11:26*, "Naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele. Je! Unayasiki hayo?*"

Mwili huu tulionao haukukusudiwa kuwa sehemu ya makazi ya nafsi. Ni mapenzi ya Mungu kwamba tunatumia umilele pamoja naye mbinguni.

Je umewahi kufikiria jinsi Ayubu alivyokuwa tayari kushughulikia na mateso na bahati mbaya ambayo Shetani aliweka? Ayubu 29:18*, "Ndipo niliposema, nitakufa ndani ya kioto change, name nitaziongeza siku zangu kama mchanga."*

Ayubu alikuwa tayari kuvumilia vyote alivyoweza kwa sababu alijua maisha haya ni mafupi, na baada ya maisha haya angeweza kuishi milele bila maumivu.

Ndugu zangu, je mnajua umilele una muda gani?

- Historia ya mwanadamu katika dunia ni kati ya miaka 6,000.
- Kipindi cha mababu kilianza kati ya miaka 4000 B.C.
- Ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu ilikuwa kati ya miaka 2000 B.C.
- Siku ya Pentekoste (wakati kanisa lilivyoanzishwa) ili kuwa miaka 30 A.D.
- Na wakati wa mkristo sasa ni umri wa miaka 1981 (katika 2011).
- Yote katika yote, historia ya mwanadamu ni kati ya miaka 6,000.

Kumbuka Ayubu alisema kwamba baada ya maisha haya uhai wake utazidishwa kama mchanga.

Zaburi 90:10, *"Siku za miaka yetu ni miaka sabini, na ikiwa tuna nguvu miaka themanini; na kiburi chake ni taabu na ubatili, maana chapita upesi tukatokomea mara."*

Mifungo mitatu na kumi ni miaka 70; mifungo minne ni miaka 80. Wengine wanaishi chini ya kiwango hicho; wachache wanaishi hadi miaka 100.

Hebu tuchukulie jiwe moja la ka mchanga inawakilisha siku moja ya maisha yako na unaishi miaka 80; hiyo ni mawe 80 ya mchanga. Kama ungeambiwa kubeba mchanga 80 katika mikono yako, je ungegundua jinsi yalivyo mazito sivyo? Pumzi ndogo tu inaweza kuipuliza kutoka mikononi mwako.

Kwa ajili ya mazungumzo, tuseme inchi la umbo wa msatatili mmoja la mchanga ilikuwa na vimchanga vidogo vidogo 6000, au siku 6000. Mita moja ingekuwa na 10,368,000 vimchanga vidogo vidogo. Hivyo siku za mchanga mwingi ungeweza kuwa miaka 28405.

Kama ukifikiria mchanga wote katika bahari zote (jumlisha mchanga wote wa kwenye inch kavu!) ya ulimwengu, akili haiwezi kujua idadi ya miaka inayoweza kuwa.

Kama kila mchanga mmoja unawakilisha siku moja, mchanga wote ulimwengu hauwezi kulinganisha idadi ya muda katika umilele! Mbingu au kuzimu.

Raha ya dhambi kwa ajili ya sababu kuwa ni bahati mbaya huwezi kujitoa kwa ajili ya umilele.

Ayubu 29:18, *"Ndipo nikasema nitakufa ndani ya kioto change, name nitaziongeza siku zangu kama mchanga."*

Hivyo ndivyo Ayubu alikuwa tayari kushinda kila kitu ambacho Shetani alimrushia. Kiwango cha kawaida cha uhai wa mwanadamu ni kama mchanga 70. Hakika hii siyo kitu ukilinganisha na umilele!

Raha yote ya maisha haya, hayana uthamani wa umilele katika jehanamu. Lakini, fikiria, ndugu na dada, kuhusu umilele mbinguni. Hiyo itakuwa vizuri kiasi gani!

Mbingu

Mbingu ni sehemu ya milele iliyoahidiwa na Yesu. Yoh. 14:2-3, *"Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo , ningaliwaambia, maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu, ili nilipo mimi, nanyi mwepo."*

Yesu hakuishi ndani ya nyumba alipokuwa duniani. Math. 8:20, *"Yesu akamwambia, Mbweha wana pango, na ndege wa angani wana viota; lakini Mwana wa Adamu hana mahali pa kulaza kichwa chake."*

Lakini nyumba iliyoundwa na kujengwa na fundi wa mbinguni atakuwa kamilifu kwa furaha, amani, na furaha ya watu wa Mungu. Mbingu ni sehemu isiyo linganishwa kwa uzuri.

Hakuna sehemu yoyote katika huu ulimwengu ulio zeeka inaweza kungana na mbingu.

Ufu. 21:1-22:6, *"Kisha nikaona mbingu mpya na ichi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na inchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena. Name nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari kama bibi arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe. Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena, kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita. Na yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi akasema, Tazama, nayafanya yote kuwa mapya. Akaniambia andika ya kwamba maneno hayo ni amini na kweli. Akaniambia imekwisha kuwa. Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Mimi nitampa yeye mwenye kiu, ya chemchemi ya maji ya uzima bure. Yeye ashindaye atayarithi haya, name nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu. Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili. Akaja mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na vile vitasa saba vilivyo jaa yale mapigo saba ya mwisho, naye akanena name akisema, Njooni huku name nitakuonyesha Yule Bibi arusi mke wa Mwana kondoo. Akanichukua katika Roho mpaka mlima mkubwa, mrefu akanionyesha ule mji mtakatifu, Yerusalemu ukishuka kutoka mbinguni kwa Mwenyezi Mungu, na mwangaza wake ulikuwa mfano wa kito chenye thamani nyingi kama kito cha yapsi, safi kama bilauri; ulikuwa na ukuta mkubwa mrefu, wenye milango kumi na miwili, na katika ile milango malaika kumi na wawili, na majina yameandikwa ambayo ni majina ya kabila kumi na mbili za Waisraeli. Upande wa mashariki milango mitatu, na upande wa kaskazini milango mitatu, na upande wa kusini milango mitatu, na upande wa magharibi milango mitatu. Na ukuta wa mji ulikuwa na misingi kumi na miwili na katika ile misingi majina kumi na miwili ya wale mitume kumi na wawili wa*

Mwana-Kondoo. Na yeye aliyesema name alikuwa na mwanzi wa dhahabu, apate kuupima huo mji, na milango yake, na ukuta wake. Na ule mji ni wa mraba, na marefu yake sawasawa na mapana yake. Akaupima mji kwa ule mwanzi; ulikuwa kama maili elfu na mia tano; marefu yake na mapana yake na kwenda juu kwake ni sawasawa. Akaupima ukuta wake, ukapata tharaa mia moja na arobaini na nne, kwa kipimo cha kibinadamu, maana yake cha malaika. Na majenzi ya ule ukuta wake yalikuwa ya yapsi, na mji ule ulikuwa wa dhahabu safi, mfano wa kiosafi. Na misingi ya ukuta wa mji ilikuwa imepambwa kwa vito vya thamani vya kila namna. Msingi wa kwanza ulikuwa yapsi; wa pili yakuti samawi; wa tatu kalkedoni; wan ne zumaridi; wa tano sardoniki; wa sita akiki; wa saba krisolitho; wa nane zabarajadi; wa kenda yakuti ya manjano; wa kumi krisopraso; wa kumi na moja hiakintho; wa kumi na mbili amethisto. Na ile milango kumi na miwili ni lulu kumi na mbili, kila mlango ni lulu moja. Na njia ya mji ni thahabu safi kama kioo kiangavu. Name sikuona hekalu ndani yake; kwa maana Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana Kondoo, ndiyo hekalu lake. Na mji ule hauhitaji jua wala mwezi kuangaza, kwa maana utukufu wa Mungu huutia nuru, na taa yake ni mwana kondoo. Na mataifa watatembea katika nuru yake. Na wafalme wan chi huleta utukufu wao ndani yake. Na milango yake haitafungwa kamwe mchana; kwa maana humo hamna usiku. Nao wataleta utukufu na heshima ya mataifa ndani yake. Na ndani yake hakitaingia kamwe cho chote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha mwana kondoo. Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana Kondoo. Katikati ya njia kuu yake. Na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda aina kumi na mbili, wenye kuto matunda yake kila mwezi, na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa. Wala hapatakuwa na laana yoyote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana Kondoo kitakuwamo ndani yake. Na watumwa wake watamtumikia; nao watamwona uso wake, na jina lake kita kuwa katika vipaji vya nyuso zao. Wala hapatakuwa na usiku tena, wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele. Kisha akaniambia maneno haya ni amini na kweli. Naye Bwana Mungu war oho za manabii, alimtuma malaika wake kuwaonyesha watumwa wake mambo ambayo hayana budi kuwako upesi."

Hiyo inaenda kuwa sehemu nzuri kwa waaminifu.

Uvuvio Wa Kimbingu

Vitu vingi vinavyoonekana vya asili, ambavyo Mungu aliviumba, imevuvia mamilioni ya wasafiri wenza- katika dunia hii.

Hivyo, maneno yote yasiyolinganishwa katika maneno ya kuongea, inafunua kwa ndimi za wanenaji, kupakwa na msanii hakika itazungumzia jinsi mbingu ilivyo.

Watu wengi watakuwa pale. Ufu. 7:9-10, *"Baada ya hayo nikaona na tazama, mkutano mkubwa ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa,na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao; wakilia kwa sauti kuu wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana Kondoo."*

Hitimisho

Ninawauliza, je mnataka kwenda mbinguni?

Kama mbingu siyo makazi yako, basi motoni inaweza kuwa.

Napanga kwenda mbinguni, vipi kuhusu wewe?